

# UNIVERSITY OF KABIANGA

## KITENGO CHA KISWAHILI

### MTIHANI MKUU

### MUHULA WA KWANZA

### MWAKA WA MASOMO 2016/2017

KIS 315: KISWAHILI LITERARY DEVICES AND CRITICISM

#### MAAGIZO: JIBU MASWALI MATATU. SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

- ✓ 1. a )Eleza athari ya mandhari katika utunzi wa fasihi. (Alama 5)
- b )Kazi za kifasihi haziwezi kuangaliwa vingine ila kifani na kimaudhui peke yake. Jadili kauli hii. (Alama 10)
- c )Riwaya ya *Babu Alipofufuka* ya Said A. Mohamed ina maoni gani kuhusu ujenzi wa jamii mpya huku kwetu Afrika. (Alama 15)
- ✓ 2. Tanzu za fasihi simulizi hutofautishwa kifani. Fafanua kauli hii huku ukitoa mifano maridhawa. (Alama 20)
- ✓ 3. Chambua shairi la ‘Mvumi’ kwa kuangalia vipengele vya lugha vinavyofaulisha ujumbe katika shairi. (Alama 20)
- ✓ 4. Chagua riwaya yoyote uliyosoma katika kozi hii na ufanue aina tano za wahusika wanaopatikana humo. (Alama 20)
- ✓ 5. Kwa kurejelea kazi ya *Babu Alipofufuka* ya Said A. Mohamed, jadili mbinu tano za lugha alizotumia mwandishi . (Alama 20)

## MVUVI

Ndimi mvuvi halisi, kulla vuvi nalijuwa  
Nivuwaye mikambisi, na papa wenye khatuwa  
Wala sivui vingisi, mishipi haisumbuwa  
Nimekwambiya elewa

Sivuwi bahari ndogo, hatia nanga fuoni  
Havisimbika vigogo, vilivyozama majini  
Na wala sivuwi ngogo, vidagaa na mbinini  
Siwauwi asilani

Jabali hulijilisi, jishipi nikalitupa  
Haotea mifulusi, na nguru na mijipapa  
Si kasikazi si kusi, khabari yangu nakupa  
Wala sivui kwa pupa

Na nivuapo malema, huingia ndanindani  
Maji yangu ni ya pima, thalatha u thalathini  
Na ndiyo ninayozama, lema halibwaga tini  
Uliza mimi n'nani

Na nivuapo maziyo, mavuvi ya kizamani  
Kwa hino hali niliyo, huvua kwa kutamani  
Hatafuta kiteweyo, cha wali mwema kombeni  
Haandaa siniani

Ela uvuvi wa juya, kuvua siutamani  
Sababuye 'takwambiya, ufahamiwe mwendani  
Ni kwambakwe huingiya, samaki wasothamani  
Kama wewe mwafulani

Ni kuu yangu bahari, elewa sana elewa  
Huko hakwendi vihori, wala vyenu vimashuwa  
Shoti nahodha hodari, kisha ende kwa ngalawa  
Na milango kuijuwa

Ustadh Ahmad Nassir, *Malenga wa Mvita*(1971)